WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

CHUO CHA UALIMU MAMIRE

E-mail:mamiretc@gmail.com
principal@mamiretc.ac.tz
Website:www.mamiretc.ac.tz

S.L.P 561
Babati - Manyara

Unapojibu Tafadhali taja:-
Kumb.Na.MMR/TC/UTA/02/25 **20 Agosti, 2018**

Ndg/Bi ……

S.L.P ……

……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU MWAKA 2018/2019

1.0 **UTANGULIZI**

Ninafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na mafunzo ya Ualimu kozi (Programu) ya _____ katika chuo hiki. Chuo cha Ualimu Mamire kipo kata ya Mamire, Wilaya ya Babati, Mkoa wa Manyara, umbali wa Kilometa 15 Kaskazini Mashariki ya mji wa Babati. Wanachuo wanaojiunga na chuo hiki huchaguliwa kwa kuzingatia vigezo rasmi vya ufaulu katika mtihani wa kidato cha IV na VI vilivyowekwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Chuo kinakupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na mafunzo ya Ualimu katika chuo hiki; ***hongera sana***.

2.0 **TAREHE YA KUANZA MAFUNZO**

Mafunzo kwa wanachuo wa mwaka wa kwanza yataanza tarehe **4 Oktoba, 2018.** Ripoti chuoni siku hiyo kwa ajili ya usajili na kuanza rasmi mafunzo. Mara ufikapo chuoni fuata taratibu za usajili ukiwa na vyeti halisi na viambatanisho vyote.

3.0 **HUDUMA MUHIMU**

3.1 **CHAKULA:** Wanachuo wote hupatiwa chakula chuoni katika bwalo la chakula. Chuo hakina uwezo wa kutoa huduma ya chakula maalum (special diet) kwa wanachuo wenye uhitaji huo. Aidha kila mwanachuo anatakiwa kuwa na vyombo vya chakula kama vile sahani, bakuli, kikombe na kijiko; ***vyombo vya plastiki haviruhusiwi***.

3.2 **AFYA:** Chuo kipo karibu na kituo cha afya Mamire ambapo mwanachuo anaweza kupata huduma ya matibabu kwa gharama nafuu. Matibabu zaidi hupatikana katika hospitali ya

mji wa Babati au Hospitali ya rufaaa ya Mkoa wa Manyara kwa gharama za mwanachuo mwenyewe. Hivyo iwapo una kadi ya bima ya Afya unashauriwa kuja nayo. Wanachuo wasio na Bima ya afya wanashauriwa kujiunga na huduma hiyo.

3.3 HUDUMA ZA BENKI: Huduma za benki zinapatikana mjini Babati katika matawi ya benki ya NMB, NBC na CRDB. Uongozi wa chuo unashauri wanachuo wahifadhi fedha zao benki au kwa kutumia huduma za fedha zitolewazo na makampuni ya simu kama vile M-Pesa.

3.4 USAFIRI: Usafiri wa kufika chuoni kutoka mjini Babati unapatikana kwa urahisi kuanzia saa 2:30 asubuhi hadi saa 12:00 jioni. Kuna usafiri wa bodaboda kutoka kituo cha daladala Mamire hadi chuoni kwa Shilingi 1,000 tu.

3.5 MALAZI: Malazi yanapatikana bure katika mabweni ya chuo. Unatakiwa kuleta vifaa vifuatavyo kwa ajili ya matumizi binafsi bwenini:-

(i) Shuka tatu – Light blue;
(ii) Mto na foronya mbili – Light blue;
(iii) Blanketi;
(iv) Godoro futi $2\frac{1}{2} \times 6$;
(v) Chandarua cha mviringo;
(vi) Ndoo ya maji yenye ujazo wa lita kumi (10lt) kwa matumizi binafsi;
(vii) Sanduku imara lenye kufuli kwa utunzaji salama wa vifaa vyako.

4.0 VYETI NA VITAMBULISHO

4.1 Wanaojiunga na mafunzo ya **Astashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi** wanatakiwa kuleta vyeti/hati zifuatazo:-

(i) Cheti halisi cha kidato cha nne (IV) kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA). Result slip hazikubaliki isipokuwa kama vyeti bado havijatolewa;
(ii) Cheti halisi cha kidato cha sita kama umehitimu ngazi hiyo ya Elimu;
(iii) School leaving certificate ya kidato cha nne iwapo umehitimu Kidato cha IV kabla ya mwaka 2009;
(iv) Cheti cha kuzaliwa;
(v) Barua ya mwajiri kukuruhusu kuja mafunzoni ikiwa wewe ni mwajiriwa;
(vi) Medical Examination form iliyojazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali; fomu imeambatanishwa. Hakikisha unafanyiwa vipimo vya afya vilivyoagizwa;
(vii) Vyeti vya mafunzo mengine uliyopitia;
(viii) Nakala za vyeti vya kitaaluma vilivyotajwa hapo juu.

4.2 Wanaojiunga na mafunzo ya **Stashahada ya Ualimu Elimu ya Sayansi na Hisabati** wanatakiwa kuleta vyeti/hati zifuatazo:-

(i) Vyeti halisi vya kidato cha nne (IV) na Sita (VI) vilivyotolewa na Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA). Result slip hazikubaliki isipokuwa kama vyeti bado havijatolewa;
(ii) School leaving certificate ya kidato cha IV na VI iwapo umehitimu kabla ya mwaka 2009;

(iii) Cheti cha kuzaliwa;
(iv) Barua ya mwajiri kukuruhusu kuja mafunzoni ikiwa wewe ni mwajiriwa;
(v) Medical Examination form iliyojazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali; fomu imeambatanishwa. Hakikisha unafanyiwa vipimo vya afya vilivyoagizwa;
(vi) Vyeti vya mafunzo mengine uliyopitia;
(vii) Nakala za vyeti vya kitaaluma vilivyotajwa hapo juu.

5.0 GHARAMA ZA UENDESHAJI

Kila mwanachuo anatakiwa kuchangia gharama za uendeshaji kama ifuatavyo:-

a) Ada: Ada ya mafunzo ni **TSh.600,000/=** kwa mwaka. Ada hii inaweza kulipwa yote au kwa awamu mbili; **TSh.300,000/=** kwa muhula. Malipo ya ada yafanyike mwanzo wa muhula kupitia akaunti namba **40710011348** yenye jina **Mamire Teachers College Revenue A/C** iliyopo benki ya NMB.
b) Michango:
(i) Kitambulisho **TSh.5,000/=** kwa mwaka wa kwanza;
(ii) Usajili **TSh.5,000/=** inalipwa mara moja kwa mwaka wa kwanza;
(iii) Serikali ya wanachuo **TSh.5,000/=** kwa mwaka;
(iv) Tahadhari **TSh.20,000/=** kwa mwaka;
(v) Usafi na miundombinu **TSh.20,000/=** kwa mwaka;
(vi) ICT **TSh.20,000** kwa mwaka;
(vii) Ulinzi **TSh.15,000/=** kwa mwaka;
(viii) Elimu ya Michezo **TSh.10,000/=** kwa mwaka;
(ix) Huduma ya kwanza **TSh. 5,000/=** kwa mwaka;
(x) Taaluma **TSh. 50,000/=** kwa mwaka;
(xi) Ada ya Mtihani **TSh.50,000/=** kwa wale wanaofanya mtihani wa Taifa (wanachuo wa mwaka wa pili);
(xii) Bima ya Afya **TSh.50,400/=** kwa mwaka kwa wasio na Bima ya Afya;
(xiii) T-Shirt yenye nembo ya Chuo TSh.15,000/= inapatikana chuoni;
(xiv) Mahafali mtajulishwa kulingana na mahitaji.

Michango yote ilipwe kupitia akaunti namba **40710011350** yenye jina **Mamire Teachers College Reccurent A/C** iliyopo benki ya NMB.

NB: ***Malipo yafanyike katika akaunti zilizotajwa hapo. Majina kamili ya mwanachuo yaandikwe katika fomu ya malipo(Pay-in- Slip).***

6.0 SARE ZA CHUO

Wanachuo wote lazima wavae sare rasmi ya chuo wakati wa masomo, shughuli rasmi na wakati wa matembezi nje ya chuo. Kila mwanachuo anatakiwa kuwa na sare kama ifuatavyo:-

a) Wanaume

(i) Suruali mbili rangi nyeusi plain – kitambaa imara kisichopauka haraka (kisiwe kitambaa cha kuteleza);
(ii) Koti jeusi - kitambaa imara kisichopauka haraka (kisiwe kitambaa cha kuteleza);
(iii) Mashati mawili mikono mirefu – rangi nyeupe, yenye vishikizo/vifungo vilivyoshonewa.
(iv) Tai ndefu nyeusi;
(v) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na Kamba; vyenye visigino vifupi.
(vi) Soksi nyeusi;
(vii) Mkanda wa suruali mweusi.

Mashono ya suruali na koti yazingatie picha Na.1 na 2 kama inavyoonekana hapo chini. Mitumba hairuhusiwi.



Picha namba 1



Picha Namba 2

b) Wanawake
(i) Sketi mbili nyeusi - kitambaa imara kisichopauka haraka (isiwe kitambaa cha kuteleza). Sketi iwe ya heshima, isiyobana na iwe na urefu wa sentimeta 10 chini ya magoti;
(ii) Koti jeusi - kitambaa imara kisichopauka haraka (isiwe kitambaa cha kuteleza);
(iii) Mashati mawili mikono mirefu – rangi nyeupe, yenye vishikizo/vifungo vilivyoshonewa.
(iv) Tai fupi rangi nyeusi;
(v) Viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba vyenye visigino vifupi;
(vi) Soksi nyeupe, ndefu;
(vii) Ushungi mweupe usiokuwa na urembo kwa wasichana Waislamu watakaopenda kuvaa;

Mashono ya sketi na koti yazingatie mchoro namba 1 na picha Na.3 hapo chini

Mchoro namba 1



Picha namba 3

7.0 **VIFAA VYA USAFI**

Kila mwanachuo alete

(i) Ndoo yenye ujazo wa lita 10;
(ii) Jembe lenye mpini;
(iii) Rubber Squeezer;
(iv) Mopper;
(v) Fagio wa chelewa;
(vi) Soft broom;

Vifaa hivyo vikabidhiwe ofisi ya msajili unapofika chuoni.

8.0 **VIFAA VYA TAALUMA**

(i) Daftari 13 quire 3, Kalamu za kutosha, Rrula na faili 13;
(ii) 'Mathematical instruments' seti moja (1);
(iii) Wanachuo wa kozi ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Sayansi na Hisabati waje na Scientific Calculator;
(iv) Kalamu za rangi mbalimbali kwa ajili ya kuchorea vielelezo vya kufundishia;
(v) Bunda moja la karatasi za 'photocopy' A4 (kwa mwaka) – Kabidhi kwa msajili wa wanachuo.

9.0 **NGUO ZA MICHEZO**

a) Tracksuit – dark blue;
b) Viatu vya michezo (raba);
c) T-Shirt isiyo na maandishi yoyote;
d) Bukta isiyo na maandishi yoyote;

10.0 **PICHA**: Leta picha nne (4)"passport size" Light blue background" kwa ajili ya matumizi ya ofisi.

11.0 **KANUNI NA SHERIA ZA CHUO**

Chuo cha Ualimu Mamire kama ilivyo vyuo vingine vya Ualimu, huendeshwa kwa kufuata sheria mbalimbali za nchi, kanuni, taratibu na sheria za chuo. Ukifika chuoni utapewa maelekezo kuhusu sheria za chuo pamoja na kujaza fomu ya kukubaliana na sheria hizo.

12.0 **MWISHO**

Kumbuka kuwa siku zote mwalimu anapaswa kuwa mfano bora wa kuigwa kwa mazuri na wanafunzi wake na jamii kwa ujumla. Kwa hiyo kila mwanachuo anapaswa kuzifahamu, kuzingatia na kuzifuata ipasavyo sheria za nchi, kanuni na taratibu mbalimbali za chuo. Aidha kila mwanachuo anatarajiwa kuwa na bidii katika taaluma.

Karibu sana chuo cha Ualimu Mamire.

Nada T. Nyabas
MKUU WA CHUO

GOVERNMENT OF TANZANIA

PART A: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

From: The Principal,
Mamire Teachers' college,
P.O.Box 561,
BABATI - MANYARA

To: The Medical Officer

……

……

REF: Mr/Mrs/Miss **…..……..**

(Name in full)

A. Please examine the above named as to *his/her physical and mental fitness for a full time teachers training course. The examination should include the following categories (I-III). Each category of which will render the applicant ineligible in case of defect. Pregnancy (category IV) will also render a female candidate ineligible for the course, including category V :

I. (A) Eye sight
(B) Hearing
(C) Speech
(D) Limbs
(E) Venereal disease
(F) Leprosy
(G) Peptic ulcers
(H) Epilepsy
(I)Tuberculosis

II. Neuroses

III. Others serious Diseases

IV. Pregnancy

V. Mental and Physical Fitness

PART B

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the above named and consider that *he /she is physically *fit/unfit for a full time teachers training course.

(I) (A) Eye sight……. **(E) Venereal disease……..**

(B) Hearing…… **(F) Leprosy……....**

(C) Speech……...……... **(H) Peptic ulcers……**

(D) Limbs……..... **(I) Tuberculosis…….**

(II) Neuroses ……

(III) Other serious Disease(s) …….

……

(IV) Pregnancy…….

(V) Mental and Physical Fitness ……

Name……...… Designation

…… Station……...….. Signature

…….....

Date: ……..... Official stamp:

*****Delete whichever inapplicable